

**WAKALA WATAIFA WA UTAFITI WA NYUMBA BORA NA VIFAA VYA
UJENZI (NHBRA)**



TANGAZO LA MNADA

Wananchi mnatangaziwa kwamba NHBRA itauza kwa njia ya mnada wa hadhara gari moja lililoko ofisi ya Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA), Mwenge Barabara ya Sam Nujoma Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Tarehe ya mnada huo ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:-

TAREHE	KITUO	AINA YA MALI
02/07/2016	Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi - Mwenge	NISSAN PATROL STATION WAGON

MASHARTI YA MNADA:

1. Gari itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipia papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari alilonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa gari husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua gari alilonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
4. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika yaani tarehe (30/06/2016 na 01/07/2016).
5. Mnada utaanza saa nne (04.00) asubuhi katika ofisi za NHBRA zilizopo Mwenge barabara ya Sam Nujoma mita 400 kutoka barabara ya Bagamoyo kuelekea Mlimani City.

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
**WAKALA WA TAIFA WA UTAFITI WA NYUMBA BORA NA VIFAA VYA
UJENZI**

